THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/2 **KISWAHILI 2**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

*Muda: Saa 3* **2007 Februari, 14 Jumatano Asubuhi**

---

*MAELEKEZO*

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano** (5) kwa kuchagua swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba** yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

### FASIHI KWA UJUMLA

1. Jadili matatizo yanayoikabili Fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania.

2. "Semi ni tungo za kifasihi zenye kutumia picha, tamathali na ishara" Eleza ni aina gani ya semi na vipengele vinavyounda semi zifuatazo:

   (a) Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa.

   (b) Mla mla leo, mla jana kala nini.

   (c) Uwike usiwike kutakucha.

   (d) Blanketi la babu lina chawa.

   (e) Jogoo la shamba haliwiki mjini.

3. Eleza maana na dhima ya mwandishi wa kazi ya fasihi kwa wananchi wa Tanzania.

## SEHEMU B (alama 20)

### USHAIRI

| | |
|---|---|
| **Kimbunga** | - H. Gora |
| **Mapenzi Bora** | - S. Robert |
| **Chungu Tamu** | - T.A. Mvungi |
| **Wasaka Tonge** | - M.S. Khatib |

4. Kwa kutumia vitabu **viwili (2)** vya ushairi kati ya vilivyoorodheshwa, eleza jinsi wahusika walivyotumiwa kufikisha ujumbe.

5. "Mapenzi hutawala mwili mzima wa binadamu, humkosesha macho, akili, fahamu na usikivu". Thibitisha hoja hiyo kwa kutumia vitabu **viwili (2)** vya ushairi kati ya vilivyoorodheshwa.

6. Eleza mienendo isiyokubalika ya kibinadamu katika taratibu za maisha yake ya kila siku katika diwani **mbili (2)** ulizosoma.

## SEHEMU C (alama 20)

### RIWAYA

| | |
|---|---|
| **Janga Sugu la Wazawa** | - Gabriel Ruhumbika |
| **Barua Ndefu Kama Hii** | - Mariama Ba |
| **Pesa Zako Zinanuka** | - Ben R. Mtobwa |
| **Vuta N'Kuvute** | - Shafi Adam Shafi |

7. "Sio TAMWA peke yake, hata waandishi wa riwaya wapo katika harakati za kumkomboa mwanamke". Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia vitabu **viwili (2)** vya riwaya ulivyosoma.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

8. "Dhamiri ya mtu inao mchango mkubwa katika ushindi wa mtu". Jadili hoja hiyo kwa kutumia riwaya **mbili (2)** ulizosoma.

9. "Uwezo wa kiuchumi na madaraka vimekuwa vikitumiwa kupokonya haki za raia wa tabaka la chini". Kwa kutumia mifano jadili tamko hilo ukizingatia kazi za wasanii wawili.

## SEHEMU D (alama 20)

## TAMTHILIYA

**Kwenye Ukingo wa Thim** - E. Hussein
**Morani** - E. Mbogo
**Kivuli Kinaishi** - S. Mohamed
**Nguzo Mama** - P. Muhando

10. Dhana ya kicheko inaibua hisia mbalimbali kwa wanajamii. Onesha ukweli wa kauli hiyo ukirejea katika tamthiliya **mbili (2)** zilizoorodheshwa.

11. Masikitiko ni hali ambayo inatawala katika baadhi ya tamthiliya. Fafanua kazi **mbili (2)** za tamthiliya ulizosoma kati ya zilizoorodheshwa zinazoonesha hali hiyo.

12. Eleza matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi yanayojidhihirisha katika kujenga kazi **mbili (2)** za wasanii wa tamthiliya.

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

13. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Halizuki somo bora, kuliko makosa yetu,
Kosa halina sogora, hulitenda kila mtu,
Zingatia kwa imara, kukosa tabia kwetu.

Kosa likija mapema, kuongoka si vigumu,
Hutengeza mambo vema, utakayo yakatimu,
Hapana kurudi nyuma, na kulegeza hatamu.

Kosa hukuza fikra, na mnyama kuwa mtu,
Kisha huamsha mara, bidii na ari zetu,
Ria zetu hudorora, mpaka tukose kitu.

Kila kiumbe lazima, kosa lake kufahamu,
Ya kuwa ni sura njema, asome aihitimu,
Ndipo awapo mzima, fahamu kuwa timamu.

Makosa yakitukera, ndipo tuzukapo watu,
Na uwezo na busara, kutafuta cheo chetu,
Tukapigana kwa ghera, ushindi ukawa wetu.

Njoo mapema lawama, mwili ungali mgumu,
Usije nina kilema, nimetokwa nafahamu,
Njoo ningali mzima, sijakuwa mahamumu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Makosa yana tijara, kwa kutanabahi mtu,
Kwamba ndipo ishara, ya kupigania utu,
Mpaka tutie fora, katika matendo yetu.

Kosa kitu cha daima, asiyekosa karimu,
Aliyeumba wanyama, na ndege na wanadamu,
Wenye maungo kuuma, na wa uvundo wa damu.

Makosa sikuyabera, silika ya kila mtu,
Tena yana hasara, iliyonzito kwa watu,
Walakini ni tohara, bora ya maisha yetu.

Hapa mwisho wa kilima, shairi limehitimu,
Likiwa refu si jema, halitakuwa na tamu,
Wazee wetu husoma, tungo ni ladha na hamu.

Maswali:

(a) Eleza maana ya maneno na tungo zifuatazo kama zilivyotumika katika shairi ulilosoma;

(i) Kosa halina sogora.

(ii) Zingatia kwa imara.

(iii) Utakayo yakatimu.

(iv) Tuzukapo watu.

(v) Makosa yana tijara.

(vi) Kutanabahi.

(vii) Makosa sikuyabera.

(viii) Kilima.

(ix) Ladha.

(x) Sijakuwa mahamumu.

(b) Eleza mambo **matatu (3)** yanayomfanya msanii aamini kuwa hapana somo bora kuliko makosa yetu.

(c) Kwa nini mtu hufanya makosa?

(d) Taja aina ya tamathali iliyotumika katika ubeti wa 9.

(e) Andika kichwa cha shairi hili kisichopungua maneno **matano (5)**.

14. Soma habari ifuatayo kisha eleza mbinu za kifani zilizotumika.

Chatu kubwa lilikuwa likimfukuza Maimuna. Alikimbia mbio lakini kila alipotazama nyuma, chatu lilimuandama. Alifukuzwa kwenye uwanda usio kikomo, wenye majani na maji maji yanayoteleza. Nyoka alipata kasi zaidi na Maimuna alirejeshwa nyuma. Kila mara alianguka na kujiokota mbiombio. Hata hivyo alikupuka uzuri. Pumzi zilimfoka, akahema huku moyo wake ukipiga upesi upesi. Kwa ghafla alirukia ukuta mrefu kama mnazi. Ilimbidi asite. Akatapatapa. Hajui akimbilie wapi; na nyuma chatu linakuja kama upepo.

Alipiga kelele, sasa aligeuka akalikabili chatu ----- pumzi zimemwisha ---- mwili umenyong'onyea kwa hofu na machovu. Alipiga tena kelele. Lakini chatu halikusita. Lilizidi kukimbia kama upepo. Kwa bahati chatu lilipomfikia karibu, Maimuna aliota mbawa, akawa nusu ndege; na aliruka. Chatu nalo bila mbawa liliruka. Maimuna alipomaliza ukuta, mbawa zilipukutika, na taratibu aliteremka chini. Chatu nalo lilimngoja likimeza mate tayari kumvamia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Sasa alikuwa karibu nalo zaidi. Akaligundua lilikuwa na vichwa viwili vya binadamu; vyenye sura ya babake. Chatu mtu! Akasita! Likatoa ulimi likamcheka. "Haha haha haa!. Mbio za sakafuni huishia ukingoni. Lilisema huku sauti yake ikiwa kama radi" Mbio zako zimefika wapi?

Maimuna hakuweza kujibu neno. Mdomo wake haukufumbuka. Alibaki anatetemeka. Machozi yalimviringika. Alilipigia magoti hilo joka akaomba. "Unanipigia magoti nini?" Liliuliza tena kwa kejeli. "Unisamehe usinile". Hatimaye Maimuna alijibu kwa kitetemeshi.

"Mimi babako ni kule?"

Maimuna alinyamaza kimya.

"Nisamehe" Maimuna aliinamia chini.

Muda ulipita. Maimuna alivuta hatua kutaka kumfuata baba yake, lakini ghafla, mbao za jukwaa alilokuwa amepanda zikakatika. Akatumbukia chini kwenye handaki la moto.

Ilikuwa ghafla ndipo alipoamka, kaloa jasho mwili mzima, sauti ikiwa imemkauka na mwili ukiwa umesawajika.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org